*Mulika, Juz. 44(2), 188-208*
*Jarida la Taasisi ya Taaluma za Kiswahili*
*Chuo Kikuu cha Dar es Salaam*

# Uundaji wa Maneno ya Kiswahili katika Mawasiliano Mahalia: Utafiti wa Lugha za Kundi F30

*Rehema Stephano*[1]

DOI: https://doi.org/10.56279/mulika.na44t2.3

**Ikisiri**

Uundaji wa maneno hulenga kukidhi mawasiliano kufuatia kujitokeza kwa mapengo ya mawasiliano, aghalabu, yanayosababishwa na kuzuka kwa vitu vipya au kukutana kwa makundi lugha mawili au zaidi yanayohitaji kuwasiliana na kuelewana. Makala hii inahusu uundaji wa maneno ya Kiswahili pale jamiilugha za Kundi F30, ambazo ni Wanyiramba (F31), Wanyaturu (F32) na Warangi (F33), zinapowasiliana kwa Kiswahili kwa lengo la kukidhi mawasiliano. Makala hii imeshughulikia malengo mawili ambayo ni kubainisha maneno ya Kiswahili yanayoundwa katika jamiilugha za Kundi F30 na kufafanua mbinu zinazotumika kuunda maneno hayo. Nadharia ya Usilimishaji ilitumika katika uchambuzi na mjadala wa matokeo. Mbinu zilizotumika kukusanya data ni usaili na uchambuzi matini. Matokeo ya utafiti yanaonesha kuwa, pale wazungumzaji wa lugha mahususi za Kundi F30 wanapowasiliana wao kwa wao, hutumia maneno ya asili kutaja majina hayo, lakini wanapowasiliana kwa Kiswahili, hutumia maneno ya Kiswahili yanayofahamika ndani ya kundi hilo pana. Imeonekana zaidi kuwa maneno hayo huundwa kwa kutumia kanuni nne ambazo ni unasibu, utohoaji, uhamishaji na ukarabati-maana. Kufuatia matokeo hayo, makala hii inapendekeza kwamba maneno ya Kiswahili mahalia yakusanywe na kutambuliwa kwa kuingizwa katika kamusi mahususi za Kiswahili ili jamii pana ya Waswahili iweze kunufaika nayo.

## 1.0 Utangulizi

Mawasiliano, kama ilivyo chakula na maji kwa binadamu, ni uhai wa mtu mmojammoja na jamii yoyote ile, iwe ndogo au kubwa. Hii ni kwa sababu, kupitia mawasiliano, watu huweza kukidhi mahitaji yao ya msingi. Jamiilugha mbili au zaidi zinapokutana pahala pamoja, huhitaji kuwa na lugha ya pamoja ambayo huwezesha watu wote wa jamii hizo kuwasiliana bila kipingamizi. Ili kukidhi haja hiyo, ambayo hasa hutokana na kutokea kwa mapengo ya kimawasiliano yasababishwayo, aghalabu, na kuibuka kwa vitu vipya au kukutana kwa jamiilugha mbili au zaidi zinazohitaji kuwasiliana na kuelewana, ni kawaida kwa watumiaji wa lugha katika eneo moja la kijiografia kujiundia maneno (Stephano, 2023).

[1] Profesa Mshiriki, Idara ya Lugha Kiswahili, Ndaki ya Insia na Sayansi za Jamii, Chuo Kikuu cha Dodoma.
Baruapepe: rehema.stephano2@udom.ac.tz

Mapengo ya kimawasiliano yanatokea pale makundi ya jamiilugha fulani yanapokutana na kila kundi likajikuta linapungukiwa maneno ya kutumia ili kuwasiliana na kundi lingine. Kwa hiyo, maneno huundwa ili kuziba mianya hiyo ya mawasiliano, ikiwa ni pamoja na kujibainisha na jamiilugha inayozungumza lugha ya mawasiliano mapana na kuendeleza harakati za maisha. Kwa kawaida, maneno hayo hurejelea vitu vya pamoja vilivyopo katika jamiilugha za makundi hayo. Maneno ndiyo roho ya lugha na mawasiliano kwa sababu mawasiliano hutumia zaidi msamiati kuliko vipengele vingine vya lugha (Stephano, 2020).

Kiswahili, kama lugha ya mawasiliano mapana katika nchi za Afrika, pia huundiwa maneno na vikundi mbalimbali vya kitaalamu na kijamii. Samson (1988) anabainisha maneno yaliyoundwa na mafundi wa magari kwa lengo la kukidhi matakwa yao ya kimawasiliano. Kahigi (2007) anaeleza kuhusu uundaji na uingizaji wa maneno ya Kiswahili katika programu ya kompyuta ya Ofisi ya 2003, ambapo anabainisha kuwa maneno zaidi ya 600 ya Kiswahili yalitengenezwa ili kukidhi mawasiliano ya programu hiyo. Stephano (2020) anaeleza kuhusu uundaji na matumizi ya maneno mapya ya Kiswahili katika programu tumizi ya *WhatsApp*. Anasema kuwa baadhi ya maneno hayo hayapo kwenye kamusi za Kiswahili, lakini yanatumiwa na wateja wa programu hiyo. Mifano hii itoshe kuonesha kuwa vikundi vidogovidogo ndani ya jamiilugha pana hujiundia maneno kwa lengo la kukidhi mawasiliano yake.

Uundaji wa maneno ni ujenzi au uzalishaji au utengenezaji wa maneno mapya (Lehmedi, 2021). Mchakato huu husaidia kuongeza msamiati katika lugha ili kukidhi mahitaji mapya ya mawasiliano yanayochagizwa na mabadiliko ya kiuchumi, kisiasa, kiutamaduni na kisayansi yanayotokea katika jamii (Stephano, 2020; Stephano, 2023). Mahitaji hayo ni pamoja na matumizi ya kawaida ambayo huchukua sura mpya kila siku, kutafsiri mambo kutoka lugha moja kwenda lugha nyingine, na kupata msamiati unaokubalika kulingana na shughuli na nyuga mahususi, kwa kutaja baadhi tu (Lehmedi, 2021).

Ingawa jukumu la kuunda na kusimamia uundaji wa maneno ya lugha ya mawasiliano mapana kiserikali hukabidhiwa kwa asasi maalumu (kwa Tanzania ni Baraza la Kiswahili la Taifa – BAKITA na Baraza la Kiswahili la Zanzibar – BAKIZA), watumiaji wa lugha wamekuwa wakijiundia maneno wao wenyewe bila kusubiri mamlaka. Sababu za kufanya hivyo ni kile kinachotajwa kuwa vyombo hivyo vinachelewa kutekeleza jukumu hilo.

Uundaji wa maneno ya Kiswahili usio rasmi umetumika na kutamalaki kwa muda mrefu katika eneo la Afrika Mashariki (Legère, 2006). Wazungumzaji wa Kiswahili wamekuwa wakijiundia maneno mapya ya Kiswahili kila wanapokutana na mazingira mapya kijamii, kiuchumi na kiteknolojia na kubaini ombwe la kimawasiliano na haja ya kutaka kuwa na maneno ambayo yangeweza

kuwaunganisha kimawasiliano (Legère, 2006). Legère anadai kuwa watu walipokutana na vitu/mambo mapya kutoka ughaibuni, hakuna mtu aliyewajuza majina ya vitu hivyo kwa lugha ya Kiswahili isipokuwa wao walijiundia na kuyasambaza kwa jamii pana na, mwishowe, kukubalika.

Suala la jamiilugha ndogondogo kujiundia maneno linaonesha kuwa ni vigumu kuzuia maendeleo ya Kiswahili katika nyanja na maeneo ambayo hayasimamiwi na vyombo vyenye dhamana, hususani shughuli ndogo za jamii mahususi ambazo zipo ndani ya jamii kubwa. Nchini Tanzania, mathalani, maneno ambayo watumiaji wa lugha wamejiundia yamekuwa yakikomaa na kukubalika kwa wazungumzaji wengi wa Kiswahili hata vyombo vyenye dhamana ya kukuza Kiswahili, hasa BAKITA, vinapounda maneno mengine na kuyapeleka kwa watumiaji, hupata ukinzani wa kukubalika (Legère, 2006; Philipo, 2022).

Kwa upande mwingine, pamoja na kujitahidi kuunda, kukuza na kueneza Kiswahili, vyombo vyenye dhamana hiyo vimeonekana kujihusisha na baadhi ya maeneo huku maeneo mengine yakiachwa licha ya kuwa na mchango katika kukuza na kuendeleza Kiswahili (Legère, 2006). Ismail (2021) anaongeza kuwa yapo maeneo mengine ambayo yanaweza kukuza na kuendeleza Kiswahili, lakini, ama hayajaangaliwa kwa kiasi cha kutosha au yamesahaulika.

Legère (*keshatajwa*) anapendekeza maeneo ambayo bado hayajamulikwa na yana mchango katika uundaji, ukuzaji na uendelezaji wa Kiswahili, yamulikwe. Anaendelea kusema kuwa maneno ya Kiswahili yanayoundwa katika maeneo hayo yakusanywe, yahakikiwe na kusanifishwa. Uandishi wa makala hii unaitikia wito huu muhimu. Hoja kuu ya makala hii ni kubainisha msamiati wa Kiswahili ambao umeundwa katika jamiilugha za Kundi F30 kwa lengo la kuonesha utajiri wa Kiswahili ambao haujajulikana bayana na kupendekeza uwekwe rasmi katika maandishi, hususani kamusi mahususi, ili kuinufaisha jamiilugha pana ya watumiaji wa Kiswahili. Majina hayo yanahusu masuala mahususi ya jamiilugha za kundi hilo la F30 na yanarejelea vitu vilivyopo katika jamiilugha za kundi hili na, aghalabu, ni nadra kupatikana katika jamiilugha zilizo nyingi. Vitu hivyo vinasemwa kwa Kiswahili kwa vile vinatumika hata kwa watu ambao si wazungumzaji wa lugha za Kundi F30.

Lugha za Kundi F30 zinajumuisha Kinyiramba (F31), Kinyaturu (F32) na Kirangi (F33) (Maho, 2009). Kinyiramba na Kinyaturu ni lugha zinazozungumzwa zaidi katika mkoa wa Singida. Kinyiramba kinazungumzwa katika wilaya ya Iramba na wilaya ya Mkalama, na Kinyaturu (pia Gɪrɪ̣mi/Kirimi) kinazungumzwa zaidi katika wilaya ya Singida na wilaya ya Ikungi. Kirangi kinazungumzwa katika mkoa wa Dodoma, wilaya ya Kondoa na wilaya ya Chemba.

Kinyiramba kimegawanyika katika jamiilugha zingine ndogondogo ambazo ni Kinilaamba (F31A), Kinyisanzu (F31B), Kinaushola (F31C) na Kinyambi (F31D) (Maho, *keshatajwa*). Kiniilamba kinazungumzwa katika wilaya ya Iramba katika tarafa ya Kinampanda, tarafa ya Kiomboi Bomani na tarafa ya Ruruma pamoja na wilaya ya Mkalama katika tarafa ya Kinyangiri. Kinaushola kinazungumzwa katika wilaya ya Iramba, tarafa ya Ndago; Kinyisanzu kinazungumzwa katika wilaya ya Mkalama, tarafa ya Kirumi; na Kiniambi (Kinyambi) kinazungumzwa katika wilaya ya Mkalama, tarafa ya Nduguti.

Maeneo yaliyoteuliwa katika utafiti huu yanachangia sifa nne muhimu kama zinavyobainishwa na Lüpke (2016). Mosi, maeneo hayo yapo katika ukanda mmoja wa kiisimu, yaani Kanda F, Kundi Na. 30. Pili, jamii za watu wa eneo hilo zina utamaduni unaofanana, ikizingatiwa kuwa zipo katika ukanda mmoja kijiografia (Kanda ya Kati ya Tanzania). Tatu, wanajamii wa maeneo haya wanachangamana sana kiasi cha kuweza kubadilishana vipengele mbalimbali vya lugha, yaani kuna ufanano wa kilahaja wa maneno. Nne, kuna mwingiliano wa lugha nyingi tofautofauti ambazo ni Kinyiramba, Kinyaturu na Kirangi, mbali na *lingua franka* moja tu ambayo ni Kiswahili.

## 2.0 Nadharia ya Utafiti

Uchambuzi na ufafanuzi wa data za utafiti uliozaa makala hii umeongozwa na Nadharia ya Usilimishaji ya McMahon (1994), Campbell (1998) na Winford (2003). Kama lilivyo jina lake, nadharia inaeleza kuwa jamiilugha mbili au zaidi zinapochangamana, huunganishwa na lugha moja ya mawasiliano mapana. Kwa hiyo, wazungumzaji hao hulazimika kusilimisha maneno ya lugha chanzi kwa kuyasawazisha ili yatii fonolojia na mofolojia ya lugha lengwa. Nadharia hiyo inadai zaidi kuwa usilimishaji huo haufanyiki kiholela, bali huzingatia mikakati ya kitaaluma ya uundaji wa maneno. Mikakati hiyo ni kama vile udondoshaji, upachikaji na ubadilishaji wa sauti, urefushaji wa irabu, na uwekaji wa mikazo katika maneno. Nadharia hii ni mwafaka katika utafiti uliofanyika kwa sababu unahusu makutano ya jamiilugha za Kundi F30 na jinsi jamii hizo zinavyounda maneno yanayotumika kuwasiliana pindi wanajamii hiyo wanapohitaji kuwasiliana kwa lugha pana ambayo ni Kiswahili.

## 3.0 Methodolojia

Data zilizowasilishwa na kujadiliwa katika makala hii zilipatikana kwa njia mbili ambazo ni usaili na uchambuzi matini. Mwongozo wa usaili ulikuwa na maelezo kuhusu vitu ambavyo majina yake yalikusudiwa kutajwa. Vitu hivyo vinapatikana katika jamiilugha hizo mahususi za Kundi F30 na vina majina ya Kiswahili kwa sababu vinatumika katika makutano ya watu wengi kama vile minadani, sokoni, shereheni, vilabuni, machungani na katika mahitaji mengine muhimu ya binadamu. Mtafiti aliandaa maelezo yaliyohitaji majina mbalimbali ya vitu vinavyohusishwa na unywaji, vitu vinavyohusishwa na biashara, vitu

vinavyohusishwa na ufugaji na vitu vinavyohusishwa na ujenzi. Kila mtoataarifa alikuwa na uhuru wa kutaja vitu vingi kadiri alivyoweza. Kwa vitu vya kushikika na kuonekana, maelezo yaliambatishwa na picha ya vitu hivyo.

Watoataarifa waliosailiwa walikuwa wa aina mbili. Aina ya kwanza ilihusisha wazungumzaji wazawa wa lugha za Kundi F30 ambao wanafahamu Kiswahili. Watoataarifa hao walikuwa Wanyiramba 6, Wanyaturu 4 na Warangi 8. Idadi hii iliukiliwa na utoshelevu wa data. Watoataarifa wa kundi hili waliombwa kutaja majina ya vitu kwa lugha zao za kwanza, kisha kutaja visawe vya Kiswahili vya majina ya vitu hivyo. Vilevile, walikuwa na jukumu la kufasili dhana hizo. Watoataarifa hawa walipatikana kwa njia ya usampulishaji tajwa, ambapo mtafiti alitajiwa mtoataarifa wa kwanza mwenye sifa lengwa na kiongozi wa kijiji wa eneo la utafiti.

Watoataarifa wa aina ya pili walikuwa watu wenye maarifa kuhusu isimu ya Kibantu. Hawa walikuwa wanafunzi 3 wa Shahada ya Umahiri ya Sanaa katika Kiswahili katika Chuo Kikuu cha Dodoma. Watoataarifa hawa walifafanua mbinu ambazo hutumiwa katika kuunda maneno ya Kiswahili katika jamilulugha teule. Uteuzi wa watoataarifa hao ulizingatia ujuzi wao wa masuala ya kiisimu, hasa katika uundaji wa maneno, jambo ambalo wazungumzaji wazawa wa kawaida wasingeweza kulifanya. Hawa walipatikana kwa kutumia usampulishaji lengwa wa kipekee. Kwa sababu darasa lilikuwa na wanafunzi watatu tu, ilimlazimu mtafiti kuwatumia wote katika utafiti wake.

Mbinu ya uchambuzi matini ilitumika kuhakiki majina (na maana za maneno hayo) ya Kiswahili ya vitu yaliyoundwa na kutumika katika mawasiliano mahalia ya jamiilugha za Kundi F30, ambapo kamusi mbili za Kiswahili zilihusika. Kamusi hizo ni *Kamusi ya Kiswahili Sanifu, toleo la nne* na *Kamusi Kuu ya Kiswahili, toleo la pili*. Baadhi ya maneno yaliyobainishwa yalikuwamo kwenye kamusi teule na mengine hayakuwamo. Kati ya hayo, baadhi ya maneno yaliyoswahilishwa na wazungumzaji wa lugha za Kundi F30, maana zake zilikuwa zimeboreshwa kuendana na mazingira ya watumiaji wa lugha hizo. Yale maneno ya Kiswahili ambayo hayakuwamo kwenye kamusi na yale ambayo maana zake ziliboreshwa na wazungumzaji wa lugha za Kundi F30 yamewasilishwa na kujadiliwa katika makala hii.

**4.0 Matokeo ya Utafiti**

Matokeo ya utafiti yanaonesha kuwa, katika mawasiliano mahalia ya jamiilugha za Kundi F30, maneno (katika muktadha wa makala hii, majina) ya Kiswahili huundwa ili kukidhi mawasiliano mapana ya watu wenye lugha tofautitofauti. Hata hivyo, majina yaliyo mengi hayafahamiki katika jumiilugha pana ya wazungumzaji wa Kiswahili. Majina hayo yanahusu masuala mahususi ya jamiilugha za kundi hilo la F30, yaani yanarejelea vitu vilivyopo katika jamiilugha

za kundi hili na ambayo ni nadra kupatikana katika jamiilugha nyingi nje ya kundi hilo. Vitu hivyo vinasemwa kwa Kiswahili kwa sababu vinatumika hata kwa watu ambao si wazungumzaji wa lugha za kundi hilo. Vitu hivyo hutumiwa kwenye masuala yanayowakutanisha watu wanaozungumza lugha tofauti, ikiwamo mikusanyiko ya kijamii kama sherehe na misiba pamoja na matukio ya kibiashara, yaani, sokoni, minadani na vilabuni. Kwa jumla, maeneo hayo huwakutanisha watu wanaozungumza lugha tofauti kiasi cha kulazimika kutumia lugha ya mawasiliano mapana ambayo, nchini Tanzania, ni Kiswahili.

### 4.1 Majina ya Kiswahili Mahalia katika Mawasiliano ya Lugha za Kundi F30

Uchunguzi wa lugha za Kundi F30 unaonesha kuwa majina ya Kiswahili yanayoundwa kukidhi mawasiliano ya Kiswahili mahalia yamegawanyika katika makundi manne. Nayo ni majina ya vitu vinavyohusishwa na unywaji, biashara, ufugaji na ujenzi. Maeneo yanayoundiwa maneno haya ni yale yanayokutanisha watu wa ndimi tofauti. Katika uwasilishaji wa data, maneno yenye kinyota (*) hayana visawe vyake katika Kiswahili. Kwa hiyo, neno la Kiswahili lililotolewa katika safu husika ni kisawe cha maneno mengine ya lugha za kundi F30 yaliyomo katika safu hiyo isipokuwa neno lenye kinyota. Hali hii inamaanisha kuwa jamiilugha inayotumia neno lenye kinyota, haina neno la Kiswahili linalorejelea kitajwa. Alama ya mabanoduara, yaani ( ) imetumika kuonesha maumbo ya wingi ya maneno husika. Alama ya kistari-ungio (-) inaashiria kutokuwapo kwa neno la kitajwa katika lugha teule. Vilevile, katika uwasilishaji wa data, alama ya mkwaju (/) imetumika kuonesha visawe, yaani maneno yaliyotenganishwa kwa mkwaju yana maana moja au inayokaribiana.

#### 4.1.1 Majina ya Vitu Vinavyohusishwa na Unywaji

Katika jamiilugha za kundi F30, kuna vitu na vifaa vinavyotumika katika unywaji. Vifaa hivi vina majina tofautitofauti kutoka lugha moja hadi nyingine, na, wakati mwingine, kutoka lahaja moja ndani ya lugha moja hadi nyingine. Pamoja na tofauti hizo, majina hayo, wakati mwingine, hurejelewa kwa jina moja la Kiswahili ndani ya jamiilugha moja au ndani ya Kundi F30. Jedwali Na. 1 linaonesha majina ya vitu hivyo katika lugha za kundi F30 ambavyo ni **kipeyu**, **tengere**, **makomba**, **kangara**, **magahi**, na **mtukuru**.

**Jedwali Na. 1: Majina ya Vitu Vinavyohusishwa na Unywaji**

| Na. | Kiswahili | Kinyiramba (F31) | Kinyaturu (F32) | Kirangi (F33) | Picha | Maana |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 1. | kipeyu | *kị̣ịko (vi-)/lụkuru - nkulu* | *ụkuu* | *kisuuju (vi-) lụkuru – nkulu* |  | Kifaa kinachotengenezwa kutokana na mumunye kukatwa kwa wima kuanzia juu mpaka chini, yaani mumunye moja hutoa vipeyu |

| Na. | Kiswahili | Kinyiramba (F31) | Kinyaturu (F32) | Kirangi (F33) | Picha | Maana |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | | viwili. |
| 2. | tengere (ma-) | *tyengele (ma-)/tyolo (ma-)* | *iṭengee* | *kerere* |  | Kifaa kinachotengenezwa kutokana na mumunye kukatwa kwa duara pana sehemu ya juu. |
| 3. | makomba | *shụmbị* | *ihụmbi/changa* | *itaantị* | | Chachu inayotengenezwa kwa uji wa mabaki ya ugali yaliyolowekwa kwa takribani wiki mbili, kisha kupikwa siku mbili kabla ya kutengeneza uji wa kimea cha nafaka (mtama, mahindi, uwele au ulezi) ambapo huchanganywa na uji huo ili kutengeneza pombe. |
| 4. | kangara | *nkangala* | *nkhangaa/ masakalani* | *irụsụ ra hụụkị* | | Pombe iliyotengenezwa kwa uji wa kimea cha nafaka (mtama, uwele, mahindi, ulezi), kisha kutiwa makomba na asali. |
| 5. | magahi/ magai | *magahi mankata* | *maghahị* | - | | Kinywaji kisicho na kilevi kinachotengenezwa kwa (kimea cha) mtama/ulezi. |
| 6. | mtukuru | *magahi mantụlụ (ntụlụ)* | *mụtukuru* | - | | Pombe iliyotengenezwa kwa nafaka, hasa mtama. |

**Chanzo:** Data za Utafiti (2024)

Jedwali Na. 1 linaonesha majina ya Kiswahili ya vitu vinavyohusishwa na unywaji katika jamiilugha ya Kundi F30. Vitu hivyo vina majina yake katika lugha mahususi za kundi hilo, lakini vinapewa majina ya Kiswahili ili wazungumzaji wa

lugha hizo waweze kuwasiliana na watu wengine ambao hawazijui lugha hizo ila wanajua lugha ya mawasiliano mapana ambayo ni Kiswahili. **Kipeyu (vi-)** ni *kịịko* (*vi*-)/*lụkuru* – *nkulu* (Kinyiramba), *ụkuu* – *nkuu* (Kinyaturu) na *kisuuju* (*vi*-)/lụkuru – *nkulu* (Kirangi). **Tengere** (**ma-**) ni *tyengel*e (*ma*-)/*tyolo* (*ma*-) (Kinyiramba), na *iṭengee* (*ma*-) (Kinyaturu). **Makomba** ni *shụmbị* (Kinyiramba), na *ihụmbi/changa* (Kinyaturu). **Kangara** ni *nkangala* (Kinyiramba), na *nkhangaa*/*masakalani* (Kinyaturu). **Magahi**/**magai** ni *magahi mankata* (Kinyiramba) na *maghahị* (Kinyaturu). **Mtukuru** ni *magahi mantụlụ* (*ntụlụ*) (Kinyiramba) na *mụtukuru* (*nṭui*) (Kinyaturu).


Aidha, data inaonesha kuwa kuna baadhi ya maneno yanayoweza kupatikana katika kamusi za Kiswahili kama ilivyo neno *kangara*, lakini maana zake zikaboreshwa kuendana na mazingira ya lugha teule. Suala hili linaashiria kwamba neno moja linaweza kurejelewa kwa namna tofauti kulingana na mazingira ya kimatumizi ya jamiilugha tofauti. Aidha, inaashiria kwamba neno hili linatumika katika jamiilugha pana ya Watanzania lakini maana yake inafinyangwa kulingana na mazingira ya watumiaji mahususi wa lugha.

Ingawa Nadharia ya Usimilishaji inaelekeza kusahihisha maneno yanayokopwa kulingana na fonolojia na mofolojia ya lugha lengwa, data ya Jedwali Na. 1 inaonesha kuwa usimilishaji unazingatia pia muktadha wa kitamaduni wa lugha lengwa. Hivyo, ni vema maana za maneno zilizopo kwenye kamusi za Kiswahili zikaboreshwa kwa kuongeza au kudokeza malighafi zinazohusika katika utengenezaji wa kitu fulani katika mazingira tofauti. Hata hivyo, hili linaweza kufanyika baada ya kuwapo kwa utafiti mpana kwani kuna uwezekano kukawa na tofauti ndogondogo za maana kulingana na miktadha ya jamii tofauti.

### 4.1.2 Majina ya Vitu Vinavyohusishwa na Biashara

Biashara ni moja ya shughuli zinazowakutanisha wazungumzaji wa lugha tofauti. Ingawa majina yanayohusishwa na unywaji yametajwa katika mwelekeo huo, majina hayo pia yanahusishwa na biashara. Aidha, katika jamiilugha ya Kundi F30, kuna bidhaa za kitamaduni ambazo hupelekwa sokoni. Bidhaa hizi zimeundiwa majina ya Kiswahili ndani ya jamii hizo na yanatumika pale washiriki wa biashara wanapohitaji kuwasiliana kwa Kiswahili. Baadhi ya majina ya vitu na bidhaa zinazotokana na vitu vya kitamaduni ni **sasati**/**jumbau**, **togo**, **furu**, **lade**, **kimbu** na **masesa**. Majina hayo yamewasilishwa katika Jedwali Na. 2.

**Jedwali Na. 2: Majina ya Vitu Vinavyohusishwa na Biashara**

| **Na.** | **Kiswahili** | **Kinyiramba (F31)** | **Kinyaturu (F32)** | **Kirangi (F33)** | **Picha** | **Maana** |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 1. | sasati/jumbau (ma-) | *nsisaai/ nsalati* | *sasaṭi/ntae* | *ijumbau (ma-)* |  | Tunda dogo lenye mbegu kubwa moja na ladha ya tangawizi |

| | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 2. | kimbo | *kɨɨmbo/kɨmbʉ* | *kɨmbʉ* | **kɨdeeko* | - | Kipimo cha kilogramu 1 au lita moja |
| 3. | togo(ma-) | *tyogo (ma-) itogo (ma-)* | *iţogho (ma-)* | **itwa (ma-)* |  | Tunda dogo lenye vipande vidogo kati ya vitatu hadi vitano; lina sukari na mlenda na mbegu ndogo chache |
| 4. | furu | *mpulu* | *mpuu* | *mpuru* |  | Tunda dogo jeusi ambalo lina umbo la kuchongoka na mbegu moja |
| 5. | lade | *lade/mbilu nkʉngʉlʉsuli* | *lade* | **ivirwa (ma-)* |  | Tunda dogo ambalo, aghalabu, huwa na rangi ya kahawia linapoiva/kukauka. Tunda hilo huwa na mbegu kubwa mbili ambazo huzungukwa na unga |
| 6. | masesa | *masesa/maasesa* | *masesa* | **chofea* | | Kitu cha nyongeza anachopewa mtu baada ya kununua kitu |

**Chanzo:** Data za Utafiti (2024)

Jedwali Na. 2 linawasilisha majina ya Kiswahili ya vitu vinavyouzwa katika jamiilugha za Kundi F30. Vitu hivyo vinanunuliwa na watu wanaozungumza lugha tofauti, vinaweza kuwa vya kundi hilo au lugha vya makundi mengine. Vitu hivyo vina majina yake katika lugha mahususi za Kundi F30, lakini vinaundiwa majina ya Kiswahili ili washiriki wa biashara waweze kuelewana kwa namna moja kwa sababu vinauzwa/vinanunuliwa na watu wanaozungumza lugha tofautitofauti. **Sasati**/**jumbau** (**ma-**) ni *nsisaai*/*nsalati* (Kinyiramba), *sasaţi*/*ntae* (Kinyaturu) na *ijumbau* (*ma*-) (Kirangi). **Kimbo** ni *kɨɨmbo*/*kɨmbʉ* (Kinyiramba), na *kɨmbʉ* (Kinyaturu). **Togo** (**ma-**) ni *tyogo* (*ma*-)/ *itogo* (*ma*-) (Kinyiramba), na *iţogho* (*ma*-) (Kinyaturu). **Furu** ni *mpulu* (Kinyiramba), *mpuu* (Kinyaturu) na *mpuru* (Kirangi). **Lade** ni *lade*/*mbilu*/*nkʉngʉlʉsuli* (Kinyiramba), na *lade* (Kinyaturu). **Masesa** (nyongeza) ni *masesa*/*maasesa* (Kinyiramba), na *masesa* (Kinyaturu).

Shughuli za kibiashara zinachangia sana katika uundaji wa maneno ya Kiswahili. Légere (2006) anasema kuwa, hata zilipoingia kompyuta na simu za mikononi katika eneo la Afrika Mashariki, wauzaji na wanunuzi walijitengenezea majina ya

Kiswahili yanayorejelea vifaa hivyo pamoja na vitu vinavyotumika sambamba na vifaa hivyo. Majina hayo ni kama vile *kompyuta*, *baruapepe* na *mtandao.*

Kwa jumla, matokeo ya utafiti unaoripotiwa katika makala hii yanaeleza kuwa shughuli za kibiashara zinakutanisha watu wa ndimi tofauti ambao ni lazima wawe na lugha moja ya kuwaunganisha. Lugha hiyo huambatana na uundaji wa maneno ambao, aghalabu, hutegemea malighafi za lugha zilizopo katika jamii. Malighafi hizo ni maneno ya lugha chanzi ambayo, kwa kiasi kikubwa, hutoholewa kuunda maneno ya lugha lengwa ambayo inatarajiwa kukidhi mawasiliano ya jamii pana.

### 4.1.3 Majina ya Vitu Vinavyohusishwa na Ufugaji

Shughuli za ufugaji pia zinawakutanisha watu wanaozungumza lugha tofauti. Makutano hayo yanasababishwa na kuchangia njia za kupitisha mifugo, pamoja na sehemu za kulishia na kunyweshea mifugo. Kufuatia mchangamano huo, wazungumzaji wa lugha tofauti ndani ya jamiilugha za Kundi F30 hulazimika kuunda maneno ya Kiswahili ambayo huwasaidia kuelewana wakiwa pamoja. Maneno ya Kiswahili yanayohusiana na ufugaji ni **palio** (visawe vyake ni *palilo* na *paririo*), pamoja na **mwambo** kama yanavyowasilishwa katika Jedwali Na. 3.

**Jedwali Na. 3: Majina ya Vitu Vinavyohusishwa na Ufugaji**

| Na. | Kiswahili | Kinyiramba (F31) | Kinyaturu (F32) | Kirangi (F33) | Picha | Maana |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 1. | palio/ palilo/paririo | *pyanda (ma-)/ ipanda (ma-)* | *ifanda* | *irira* |  | Njia ndefu na pana inapopita mifugo |
| 2. | mwambo | *mʉlambo/ mwambo* | *mwambo* | *mʉlambo* | - | Mtaro/mfereji kwa ajili ya kunyweshea mifugo |

**Chanzo:** Data za Utafiti (2024)


Katika Jedwali Na. 3, kuna majina ya Kiswahili ambayo yameundwa kutokana na shughuli za ufugaji. Dhana zinazorejelewa kwa kutumia majina hayo ya Kiswahili zina majina yake katika lugha za Kundi F30. **Palio** ni *pyanda* (Kinilamba, Kinaushola na Kinyambi), *ipanda* (Kinyisanzu), *ifanda* (Kinyaturu), na *irira* (Kirangi) na **mwambo** ni *mʉlambo* (Kinilamba, Kinaushola, Kinyambi na Kirangi) na *mwambo* (Kinyisanzu na Kinyaturu). Dhana hizo zimeundiwa majina ya Kiswahili ili ziweze kueleweka kwa watu wanaotumia lugha tofauti—inawezekana zikawa za kundi hili au zisizo za kundi hili—lakini mawasiliano hayo yanafanyika katika eneo la kijiografia zinapozungumzwa lugha za Kundi F30.

### 4.1.4 Majina ya Vitu Vinavyohusishwa na Ujenzi

Ujenzi hutupatia malazi ambalo ni hitaji la msingi la binadamu na mifugo. Ujenzi wa nyumba, mathalani, una mahitaji mengi kuanzia katika msingi hadi paa, na

huweza kukamilishwa na ujenzi wa uzio. Mahitaji hayo huweza kufanana kutoka jamii moja hadi nyingine. Jamiilugha za Kundi F30 zina vifaa vya ujenzi vinavyotumika katika jamii pana inayohitaji kuunganishwa kwa Kiswahili katika mawasiliano. Vifaa hivyo ni **kuruwili (ma-**) ambalo kisawe chake ni **kuluwiri** (**ma-**) na **mnyaa** (**mi-**). "Makuruwili" hutumika kupaua nyumba na kujengea uzio wa nyumba au uzio wa kibanda cha biashara na kupumzikia ambacho huweza kuezekwa kwa nyasi pia. "Mnyaa" hutumika kujengea uzio wa kaya, zizi na palio. Jedwali Na. 4 linawasilisha majina ya vifaa vya ujenzi katika jamiilugha za Kundi F30.

**Jedwali Na. 4: Majina ya Vitu Vinavyohusishwa na Majenzi**

| **Na.** | **Kiswahili** | **Kinyiramba (F31)** | **Kinyaturu (F32)** | **Kirangi (F33)** | **Picha** | **Maana** |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 1. | kuruwili /kuluwiri (ma-) | *isaanze (ma-) lembele* | *ivevee/isira (ma-)* | *kuluwiri (ma-)* |  | Mmea mrefu kama mmea wa mtama/uwele unaoota kwenye maji mengi, hususani mbugani wenye majani ma refu na unaotoa suke kama la uwele ambao hutumika kuezekea nyumba au kujengea mabanda ya kupumzika au uzio wa nyumba |
| 2. | mnyaa (mi-) | *mụụgị (mị-)/ mụnụge (mị-)/ mụnyala (mị-) -* | *mụnyaa (mị-)/inyaa (ma-)* | *ng'ondu/ mnyaa (mi-)* |  | Mti wenye matawi kama vidole ambao hutoa utomvu mweupe kama maziwa ambao hutumika kujengea uzio wa kaya, palio au zizi |

**Chanzo:** Data za Utafiti (2024)

Jedwali Na. 4 linawasilisha majina ya vitu vinavyotumika katika ujenzi kwa jamii pana ya wazungumzaji wa lugha za Kundi F30 na wazungumzaji wa lugha zingine wanapokuwa katika eneo la jamii hiyo. Dhana hizo, ingawa zinarejelewa kwa majina tofauti baina ya lugha za Kundi F30 na baina ya lugha moja mahususi ndani ya kundi hilo, zimepewa pia majina ya Kiswahili ili kuwa na neno moja la kurejelewa na watu wote wanapotumia Kiswahili bila kujali lugha zao za kwanza ambazo zina majina tofauti kuhusu dhana hizo. Katika lugha za Kundi F30, maneno yanayorejelea dhana ya **kuruwili** ni *isaanze*/*ilembele* (Kinyiramba), *ivevee*/*isira* (Kinyaturu) na *ng'ondu*/*ikuluwiri* (Kirangi). Majina yanayorejelea dhana ya **mnyaa** ni *mụụgị* (Kinilamba na Kinaushola), *mụnụg*e (Kinyambi),

*mų̣nyala* (Kinyisanzu), *mų̣nyaa (mɪ̣-)*/*inyaa (ma-)* (Kinyaturu), na *ng'ondu*/*mnyaa* (Kirangi).

Ni dhahiri kuwa ujenzi ni shughuli mojawapo inayowakutanisha watu wanaozungumza lugha tofauti na inayotumia malighafi za kuchangia, yaani zinazotumiwa na watu wanaozungumza lugha tofauti. Kwa hiyo, wazungumzaji hao wanashurutishwa kuwa na maneno ya Kiswahili ya malighafi zinazotumika katika ujenzi ili mawasiliano yaweze kufanyika na ujenzi ufanikiwe.

**4.2 Mbinu za Uundaji wa Maneno ya Kiswahili Mahalia**

Uundaji wa maneno ya lugha huhusisha mbinu mbalimbali. Matokeo ya utafiti yanaonesha kuwa uundaji wa maneno ya Kiswahili katika mawasiliano mahalia ya jamiilugha za Kundi F30 hutumia mbinu za aina nne. Mbinu hizo ni unasibu, utohoaji, uhamishaji na ukarabati-maana. Hata hivyo, uundaji wa neno moja unaweza kuhusisha mbinu zaidi ya moja.

**4.2.1 Unasibu**

Unasibu unahusu utajaji wa majina ya vitu pasipo jina kuwa na uhusiano wa moja kwa moja na kirejelewa. Jina linatajwa bila kuzingatia sifa za kitu husika. Katika data za maneno ya Kiswahili yanayotumika katika mawasiliano mahalia ya Kundi F30, kuna baadhi ya maneno yaliyoundwa kinasibu kama yanawasilishwa katika Jedwali Na. 5.

**Jedwali Na. 5: Maneno Yanaundwa kwa Njia ya Unasibu**

| Na. | Umoja | Wingi |
|---|---|---|
| 1. | kipeyu | vipeyu |
| 2. | kuruwili | makuruwili |
| 3. | palio | mapalio |

**Chanzo:** Data za Utafiti (2024)

Katika Data Na. 1, maneno ya Kiswahili yaliyoundwa hayana uhusiano wa moja kwa moja na dhana zinazorejelewa katika lugha mahususi za Kundi F30, yaani yameundwa kinasibu. Habwe na Karanja (2004) wanadai kuwa, katika uitaji wa majina, unasibu unarejelewa kama kitendo cha kuita kitu kutokana na mazoea ya wanajamiilugha husika, ambapo hakuna uhusiano wa moja kwa moja kati ya umbo na maana. Katika ufafanuzi wa majina yaliyoundwa kinasibu kwa mujibu wa utafiti uliofanyika, tuliona kuwa **kipeyu** ni kifaa kinachotengenezwa kutokana na mumunye kukatwa kwa urefu kuanzia juu mpaka chini; **kuruwili** ni mmea mrefu kama mmea wa mtama/uwele unaoota kwenye maji mengi, hususani mbugani wenye majani marefu na unaotoa suke kama la uwele; na **palio** (ambalo visawe vyake ni *palilo* na *paririo*) ni njia ndefu na pana inapopita mifugo.

### 4.2.2 Utohoaji

Lugha mbili au zaidi zinapochangamana, hulazimisha utohoaji wa maneno kufanyika ili kukidhi mawasiliano ya kundilugha moja kubwa linaloundwa na lugha hizo (Okal, 2012). Utohoaji ni kitendo cha kukopa neno kutoka lugha chanzi na kuliboresha kulingana na kaida za kifonolojia na kimofolojia za lugha lengwa. Mabadiliko yanayotokea katika utohoaji (udondoshaji, ubadilishaji na uchopekaji wa sauti) hayabadilishi maana za maneno hayo (Msuya na Mreta, 2019). Ili kuunda maneno ya Kiswahili katika mawasiliano mahalia ya lugha za Kundi F30, utohoaji unatumika kama inavyowasilishwa katika Jedwali Na. 6.

**Jedwali Na. 6: Maneno Yanaundwa kwa Njia ya Utohozi**

| **Na.** | **Umoja** | **Wingi** |
|---|---|---|
| 1. | furu | furu |
| 2. | jumbau | jumbau |
| 3. | kangara | kangara |
| 4. | kimbo | kimbo |
| 5. | magahi | magahi |
| 6. | mnyaa | minyaa |
| 7. | mtukuru | mitukuru |
| 8. | mwambo | miambo |
| 9. | sasati | sasati |
| 10. | tengere | matengere |
| 11. | togo | matogo |

**Chanzo:** Data za Utafiti (2024)

Maneno yaliyowasilishwa katika Jedwali Na. 6 yametoholewa kutoka lugha za Kundi F30. Neno **furu**, kwa mfano, limetoholewa kutoka maneno matatu tofauti, kila moja kutoka lugha moja ya Kundi F30. Maneno hayo ni *mpulu*, *mpuu*, *mpuru* kutoka Kinyiramba, Kinyaturu na Kirangi, kwa mfuatano huo. Neno **mnyaa** limetoholewa kutoka maneno *mụnyala* na *mụnyaa* ya Kinyiramba (Kinyisanzu) na Kinyaturu, kwa mfululizo huo, na neno **mwambo** limetoholewa kutoka neno *mụlambo* la Kinyiramba na Kirangi. Neno **tengere** limetoholewa kutoka maneno mawili *tyengele* na *ịtengee* ya Kinyiramba na Kinyaturu. Neno **jumbau** limetoholewa kutoka neno la Kirangi *ijumbau*. Neno **togo** limetoholewa kutoka maneno matatu ya Kinyiramba na Kinyaturu. Nayo ni *ityogo* na *itogo* kutoka Kinyiramba (Kinilamba, Kinaushola, na Kinyambi; na Kinyisanzu mtawalia) na *ịtogho* kutoka Kinyaturu.

Maneno mengine yaliyotoholewa ni **kimbo**, **magahi**, **mtukuru**, **sasati** na **masesa**. **Kimbo** ni neno la Kiswahili linalotumika katika jamiilugha za Kundi F30 kurejelea chombo kinachotumika kupimia kilogramu au lita. Neno hili limetoholewa kutoka maneno mawili ambayo ni *kịịmbo* (Kinilamba, Kinaushola

na Kinyambi) na *kịmbụ* kutoka Kinyisanzu na Kinyaturu. Neno **magahi** (kisawe chake ni magai) limetoholewa kutoka neno la Kinyaturu *maghahị*. Neno **mturukuru** limetoholewa kutoka neno la Kinyaturu *mụtukuru* lenye maana ya pombe ya asili iliyotengenezwa kwa mtama, mahindi au uwele na makomba (chachu ya kawaida) bila asali. Neno **sasati** limetoholewa kutoka maneno mawili ya Kinyiramba na Kinyaturu ambayo ni *nsalati* na *sasaṭi*. Neno **masesa** limetoholewa kutoka neno *masesa* la Kinilamba, Kinyambi na Kinyisanzu; na Kinyaturu na *maasesa* kutoka Kinaushola.

Kwa ujumla, utohoaji wa maneno kutoka lugha za Kundi F30 kwenda Kiswahili unahusisha mabadiliko ya kifonolojia na kimofolojia. Katika data, mabadiliko ya kifonolojia yamehusisha udondoshaji wa sauti, ubadilishaji wa sauti na uchopekaji wa sauti. Udondoshaji wa sauti za konsonanti na irabu umetokea katika maneno ya lugha za Kundi F30 wakati wa utohoaji wa maneno hayo kwenda Kiswahili. Udondoshaji uliofanyika ni wa aina mbili: unaozingatia kanuni za kifonolojia na usiozingatia kanuni za kifonolojia.

Udondoshaji unaozingatia kanuni za kifonolojia, kwa mujibu wa makala hii, ni ule ambao mazingira ya kuondoshwa sauti fulani katika neno yanaelezeka kwa mujibu wa kanuni za kifonolijia. Udondoshaji wa aina hii umehusisha nazali /m/ na kitambaza /l/. Nazali /m/ iliyopo mwanzoni mwa maneno *mpulu*, *mpuu*, *mpuru* kutoka Kinyiramba, Kinyaturu na Kirangi, kwa mpangilio huu, yaani inayofuatiwa na sauti /p/ imedondoshwa. Kadiri ya Olson (1964), katika Kinyaturu, mathalani, sauti /p/ na /f/ ni alofoni. Sauti /p/ hutokea katika mazingira ya kutanguliwa na kipasuo cha midomo /m/, na sauti /f/ hutokea katika mazingira ya kutotanguliwa na kipasuo hicho. Mazingira ya udondoshaji wa sauti hii yanaweza kufanana katika lugha zote za Kundi F30 kwa sababu lugha za kundi moja zinachangia sifa zilizo nyingi.

Vilevile, kitambaza /l/ kimedondoshwa katika neno la Kinyiramba (Kinyisanzu) *mụnyala* na la Kinyiramba na Kirangi *mụlambo*. Udondoshaji wa sauti /l/ unafanyika pia katika lugha nyingine za Kibantu, ambapo, mara nyingi, sauti hii inapokuwa katikati ya irabu mbili, hudondoshwa ili kurahisisha matamshi (Kiplimo na Mwita, 2021; Kiplimo, 2022).

Udondoshaji mwingine wa sauti umehusisha irabu /ụ/ katika maneno *mụnyala* na *mụnyaa* ya Kinyiramba (Kinyisanzu) na Kinyaturu, kwa mfululizo huo, na neno *mụlambo* la Kinyiramba na Kirangi, ambapo maneno **mnyaa** na **mwambo** yameundwa. Zaidi, sauti /ụ/ ilipokutana na /a/, pakazaliwa kiyeyusho /w/. Kihistoria, kiyeyusho /w/ kinatokea pale irabu ya juu nyuma inapokutana na irabu nyingine isiyofanana nayo (Mwendamseke, 2023; Stephano, 2023). Udondoshaji wa irabu /u/ au /ụ/ inayotokea katikati ya konsonanti mbili, hasa mwanzoni mwa neno, ni jambo la kawaida katika lugha za Kibantu. Stephano (2023) anadai kuwa,

katika Kinyaturu, irabu /ṷ/ inayotokea katikati ya konsonanti inayounda kiambishi awali *mu-* na konsonanti ya kwanza ya mzizi wa neno hudondoshwa katika mchakato wa uswahilishaji wa maneno.

Sauti zingine za irabu zilizodondoshwa ni /ɪ̣/ na /a/. Sauti za irabu mbili au zaidi za lugha za Kundi F30 zinapoandamana, moja hudondoshwa wakati wa uswahilishaji wa maneno hayo. Tukio hili limejitokeza katika maneno *kɪ̣ɪ̣mbo* na *maasesa* ya Kinyiramba (Kinaushola), ambapo maneno yaliyoundwa ni **kimbo** na **masesa**. Jambo hili ni dhahiri hata katika lugha zingine za Kibantu, hususani Kiswahili kama anavyodai Mgullu (1999) kuwa irabu mbili zinazofanana zikifuatana katika neno, basi irabu moja inabidi idondoshwe.

Kulingana na makala hii, udondoshaji usiozingatia kanuni za kifonolojia, ni ule ambao mazingira ya kuondoshwa sauti fulani katika neno hayaelezeki kikanuni. Udondoshaji wa sauti wa aina hii umefanyika katika maneno *tyengele* na *tyogo* ya Kinyiramba, ambapo sauti /j/ imedondoshwa. Pia, umetokea katika neno *nsalati*, ambapo sauti /n/ na /l/ zimedondoshwa. Kadhalika, katika Kinyiramba, sauti /n/ imedondoshwa katika neno *nkangala* na katika Kinyaturu, sauti /n/ na /h/ zimedondoshwa katika neno *nkhangaa*. Hafez (1996) anaeleza kuwa, wakati mwingine, udondoshaji wa sauti hauwezi kufafanulika kifonolojia wala kimofolojia, isipokuwa hulenga kusawazisha na kusahilisha tu utamkaji wa neno hilo.

Badiliko jingine la kifonolojia lililotokea katika uundaji wa maneno ya Kiswahili katika mawasiliano mahalia ya jamiilugha za Kundi F30 ni ubadilishaji ambao umehusisha sauti za aina zote mbili (irabu na konsonanti). Konsonanti zilizobadilishwa ni /p/na /f/, /l/ na /r/, /ṱ/ na /t/, na /ɤ/ na /g/. Irabu zilizobadilishwa ni /ɪ̣/ na /i/. Sauti /p/ imekuwa /f/ katika maneno *mpulu*, *mpuu*, *mpuru* pale sauti /p/ ilipotanguliwa na nazali ya mdomo /m/. Kama tulivyoona katika sehemu iliyotangulia kuhusu udondoshaji wa nazali /m/ inapotanguliwa na kipasuo /p/, katika lugha za Kundi F30, imeonekana sauti /p/ na /f/ ni alofoni kama anavyodai pia Olson (1964). Tuliona kwamba sauti /p/ hutokea katika mazingira ya kutanguliwa na kipasuo cha midomo /m/, na sauti /f/ hutokea katika mazingira ya kutotanguliwa na kipasuo hicho. Sauti /p/ na nazali /m/ zinatamkiwa mahali pamoja, yaani midomoni ndio maana zinaweza kuandamana katika neno.

Aidha, katika Kinyiramba, sauti /l/ katika maneno *mpulu* na *tyengele* imebadilishwa kwa /r/. Ubadilishaji wa sauti /l/ na /r/ ni suala la kilahaja katika Kibantu, yaani sauti moja inakuwa katika lugha moja na nyingine katika lugha nyingine au sauti zote zinakuwapo katika lugha moja, hivyo, kubadilishana nafasi, na ubadilishaji huo hauathiri maana (Kiplimo na Mwita, 2021; Kiplimo, 2022). Aidha, sauti hizi zina tabia sawa, yaani zote ni vilainishi vya ufizi (Mwendamseke, 2023).

Sauti /ț/ imebadilishwa na kuwa /t/ katika maneno ya Kinyaturu *ițengee* (tengere), *ițogho* (togo) na *sasați* (sasati)/. Ubadilishaji wa /ț/ na /t/ unaonesha kuwa sauti hizi zina tabia za kifonetiki zinazolingana. Sauti hizi zote zinatamkiwa kwenye ufizi na si ghuna. Pia, inaonekana kuwa sauti ya Kinyaturu /ț/ haipo kwenye Kiswahili ndiyo maana nafasi yake inachukuliwa na /t/ ambayo ipo katika Kiswahili.

Sauti /ɤ/ imebadilishwa kuwa /g/ katika Kiswahili kama inavyoonekana katika maneno ya Kinyaturu *ițogho* (togo) na *maghahi* (magahi/magai). Sauti hizi zote zipo katika lugha zote (Kundi F30 na Kiswahili). Hata hivyo, ubadilishanaji wa nafasi wa sauti /ɤ/ na /g/ unalenga kuteua sauti ambayo imezoeleka zaidi katika Kiswahili ambayo ni /g/. Ubadilishaji wa sauti hizi ni tukio la kawaida katika lugha za Kibantu. Bernander (2012) anadai kuwa sauti /ɤ/ hubadilishwa kwa sauti /g/ katika utohozi wa maneno kutoka Kibena kwenda Kibantu. Pia, Msuya na Mreta (2019) wanasema kwamba ubadilishanaji huu unajitokeza kwenye utohoaji wa maneno kutoka Chasu kwenda Kiswahili.

Ubadilishaji wa irabu umehusisha irabu /ị/ kuwa /i/. Sauti hizo zimebadilishwa katika maneno mawili ambayo ni *kịịmbo* (Kinyiramba) na *kịmbụ* kutoka Kinyiramba (Kinyisanzu (F31B)) na Kinyaturu. Kwa hiyo, sauti /ị/ imekuwa /i/ ambayo ipo katika Kiswahili. Ubadilishanaji wa irabu, kama ilivyo kwa konsonanti, unatokana na ukuruba wa kifonetiki uliopo baina ya sauti hizo (Mwendamseke, 2023). Irabu /ị/ ni ya juu kati mbele, wakati irabu /i/ ni ya juu mbele. Olson (1964) anaeleza kuwa irabu za Kinyaturu /i/ na /ị/ ni sawa na irabu ya Kiswahili /i/.

Uchopekaji wa sauti ni badiliko jingine linalojitokeza katika utohoaji wa maneno kutoka lugha za Kundi F30 kwenda Kiswahili. Katika neno **tengere**, ambalo limetoholewa kutoka neno la Kinyaturu *ițengee*, sauti /r/ imechopekwa. Uchopekaji wa sauti /r/ (au /l/ ambayo ni alofoni yake) katika maneno ya Kiswahili na ya Kibantu, kwa ujumla, unadumisha umbo la Mamebantu la maneno hayo (Mwita na Kiplimo, 2021). Aidha, uchopekaji umefanyika katika neno **sasati** ambalo limetoholewa kutoka neno *nsalati* la Kinyiramba baada ya udondoshaji wa sauti /n/ na /l/, ambapo sauti /s/ imewekwa katikati ya /a/ mbili. Uchopekaji huo umelenga kukidhi fonolojia ya lugha pokezi ambayo ni Kiswahili inayopendelea silabi huru, yaani mfuatano wa konsonanti na irabu dhidi ya irabu peke yake.

Badiliko jingine ni udondoshaji wa viambishi vya ngeli unaotokea kwenye maneno ya Kinyiramba *ityogo* (*ma-*) na *itogo* (*ma-*), maneno ya Kinyaturu *ițengee* (*ma-*) na *ițogho* (*ma-*), na neno la Kirangi *ijumbau* (*ma-*). Udondoshaji wa kiambishi {*i-*} unatii mofolojia ya ngeli ya nomino ya *JI-*, *Ø-/MA-* ya Kiswahili na kuachana na mofolojia ya ngeli ya *I-/MA-* ya lugha za Kundi F30. Stephano (2023) anaeleza kuwa maneno ya Kiswahili ya ngeli ya *JI-*, *Ø-/MA-* ya Kiswahili

yanapotoholewa katika Kinyaturu, hupokelewa katika ngeli ya *I-/MA-*. Kitendo hiki kinaonesha kuwa majina ya ngeli hii katika lugha za Kundi F30 pamoja na Kiswahili yana sifa moja kisemantiki. Kwa mujibu wa Kihore, Massamba na Msanjila (2012), ngeli hii inajumuisha nomino zinazohusu vitu vilivyo katika jozi, nomino za vitu ambavyo havihesabiki na nomino zinazohusu vitu vikubwa, vyenye nguvu na vyenye kuogofya. Aidha, katika Kinyaturu, nomino za aina hii zinabebwa kwenye ngeli ya RI-, I-/MA-. Kiambishi RI- kinabeba nomino zinazohusu viungo vya mwili kama vile *riho* (jicho) na *rino* (jino).

### 4.2.3 Uhamishaji

Uhamishaji wa neno ni kitendo cha kukariri au kunakili neno la lugha chanzi kama lilivyo bila kulifanyia marekebisho ya aina yoyote. Uundaji wa maneno ya Kiswahili katika mawasiliano mahalia ya jamiilugha za Kundi F30 unatumia mbinu ya uhamishaji wa maneno ya lugha chanzi katika lugha lengwa ikiwa fonolojia na mofolojia ya maneno hayo ya lugha chanzi inaendana na ya lugha lengwa. Jedwali Na. 7 linaonesha maneno yaliyoundwa kwa mbinu hizo.

**Jedwali Na. 7: Maneno Yanaundwa kwa Njia ya Uhamishaji**

| Na. | Umoja | Wingi |
|---|---|---|
| 1. | kuluwiri | makuluwiri |
| 2. | lade | lade |
| 3. | magahi | magahi |
| 4. | masesa | masesa |
| 5. | mnyaa | minyaa |
| 6. | mwambo | miambo |

**Chanzo:** Data za Utafiti (2024)

Katika Jedwali Na. 7, maneno ya lugha chanzi teule yanatumika vilevile katika Kiswahili. Katika uhamishaji, umbo la silabi, utamkaji na maana huakisiwa katika lugha lengwa na bado neno hilo likahesabika ni la lugha lengwa (Msuya na Mreta, 2019). Uhamishaji unaweza kufanyika ikiwa sauti zote za neno la lugha chanzi zipo katika lugha lengwa (Mosoto, 2016). Neno *magahi* kutoka Kinyiramba; maneno *lade* na *mases*a kutoka Kinyiramba na Kinyaturu; *mwamb*o kutoka Kinyaturu; na *kuluwiri* na *mnyaa* kutoka Kirangi yamehamishwa kama yalivyo kwenda katika Kiswahili. Hata hivyo, *magahi* ni sehemu ya kifungu cha maneno *magahi mankata* (Kinyiramba) ambacho kinamaanisha kinywaji kisicho na kilevi kinachotengenezwa kwa unga wa kimea.

### 4.2.4 Ukarabati-maana

Katika muktadha wa makala hii, ukarabati-maana ni dhana inayorejelea urekebishaji wa maana ya neno kwa kuzingatia mazingira ya jamiilugha mahususi au uga wa matumizi. Uundaji wa maneno huweza kufanyika kwa kutumia maneno yaliyopo yenye maana zake zinazotambulika, hususani kwenye kamusi za lugha

teule (Stephano, 2020). Katika mazingira hayo, maana ya neno lililopo inaweza kurekebishwa kwa kupanuliwa au kufinywa (Moses, 2019; Kibwage, 2023). Katika kujiundia maneno ya Kiswahili kwa lengo la kukidhi mawasiliano mahalia, watumiaji wa lugha katika jamiilugha za F30 wanarekebisha maana za maneno yaliyopo kwenye Kiswahili, hasa kamusini. Maneno yaliyobainika kuundwa kwa namna hii ni mawili kama yanavyowasilishwa katika Jedwali Na. 8.

**Jedwali Na. 8: Maneno Yanaundwa kwa Njia ya Ukarabati-maana**

| Na. | Umoja | Wingi |
|---|---|---|
| 1. | kangara | kangara |
| 2. | makomba | makomba |

**Chanzo:** Data za Utafiti (2024)

Maneno yaliyopo katika Jedwali Na. 8 yameundwa kutokana na kuboresha maana za maneno hayo kutoka Kiswahili ili kukidhi mahitaji ya mazingira ya mawasiliano ya lugha za Kundi F30. Katika Kiswahili, neno *kangara* lina maana ya pombe itengenezwayo kwa pumba za mahindi au mtama na kutiwa chachu na kimea cha ulezi, kisha kutiwa sukari au asali (TUKI, 2019). Katika lugha teule (Kinyiramba na Kinyaturu), neno hili linamaanisha pombe iliyotengenezwa kwa unga wa kimea cha mtama, ikatiwa makomba ambayo ndiyo chachu (*shụmbị*/*ihụmbị*), na mwisho ikatiwa asali.

Kwa hiyo, maana imeboreshwa kwa kupunguza malighafi zinazotumika kutengeneza kangara inayorejelewa katika Kiswahili ambazo ni pumba za mahindi au mtama, kimea cha ulezi na sukari. *Kangara* inayotengenezwa katika jamii za Kinyiramba na Kinyaturu inatumia unga wa kimea cha mtama na asali tu bila sukari. Kwa hiyo, umahususi wa pombe hiyo katika jamiilugha teule ni matumizi ya kimea cha mtama, makomba na asali. Pamoja na ukarabati wa maana, neno *kangara* pia lina elementi za kutoholewa kutoka katika Kibantu. Katika Kinyiramba, sauti /n/ imedondoshwa na /l/ imebadilishwa kwa /r/ na, katika Kinyaturu, sauti /n/ na /h/ zimedondoshwa na /r/ imepachikwa.

Neno jingine ambalo limeundwa kwa njia ya ukarabati-maana ni **makomba**. Katika Kiswahili, neno hili linarejelea uji wa mtama unaopikwa siku moja kabla ya kutiwa kimea ili uwe pombe (TUKI, 2019). Katika lugha teule, makomba ni chachu inayotengenezwa kwa uji wa mabaki ya ugali yaliyolowekwa kwa takribani wiki mbili, kisha kupikwa siku mbili kabla ya kutengeneza uji mwepesi wa kimea cha nafaka (mtama, mahindi, uwele au ulezi). Makomba huchanganywa na unga wa kimea ili yaumuke kwa ajili ya kuchachushia pombe.

Makomba yanayorejelewa katika Kiswahili ni uji wa mtama unaotiwa kimea ili uwe pombe, lakini katika lugha za F30 ni chachu inayotokana na uji wa mabaki ya ugali (huweza kuchanganywa na pumba za nafaka) iliyochanganywa na unga wa

kimea ili iumuke na itumike kuchachusha uji wa unga wa kimea cha nafaka kwa ajili ya kutengeneza pombe.

Ingawa wanaisimu wanadai kuwa maana za maneno yaliyopo zinaweza kupanuliwa au kufinywa wakati wa kuunda maneno mapya (Stephano, 2023; Moses, 2019; Kibwage, 2023), katika jamiilugha za Kundi F30, maana za maneno **kangara** na **makomba** hazijapanuliwa wala kufinywa. Kilichofanyika ni fasili zake kuzingatia michakato na malighafi zinazotumika kutengeneza vitu vinavyorejelewa na dhana hizo. Jambo hili linadokeza sababu ya maana za baadhi ya maneno katika kamusi kupanuliwa kwa kuongeza malighali au kudokeza kuwa kuna malighafi zingine zinazoweza kutumika kutengeneza kitu fulani kutegemea mazingira. Hata hivyo, ni dhahiri kwamba maana za maneno ya kiutamaduni zinaweza kutofautina kulingana na utamaduni wa jamii husika. Jambo hili linaondoa uwezekano wa maana zote za maneno ya kitamaduni kuakisiwa katika kamusi za jumla. Pamoja na hivyo, bado maana hizo zinaweza kuwasaidia watunga kamusi kuboresha fasili za maneno pale itakapobidi.

**5.0 Hitimisho**

Matokeo ya utafiti yamejibu kikamilifu malengo mahususi mawili yaliyoongoza utafiti uliofanyika: kubainisha maneno ya Kiswahili yanayoundwa katika jamiilugha za Kundi F30, na kufafanua mbinu zinazotumika kuunda maneno hayo. Makala imeonesha kuwa jamiilugha za Kundi F30 zina mchango unaotokana na lugha hizo kujiundia maneno ya Kiswahili kwa lengo la kukidhi mawasiliano ya jamii pana inayokutanisha watumiaji wa lugha tofauti za kundi hilo pamoja na watumiaji wa lugha zingine wanaopatikana katika maeneo zinapozungumzwa lugha hizo pale Kiswahili kinapokuwa nyenzo pekee ya kuwasiliana baina yao. Maneno hayo yanaundwa kwa kutumia mbinu nne ambazo ni unasibu, utohoaji, uhamishaji na ukarabati-maana—mbinu ya utohoaji ikiwa zalifu zaidi ikilinganishwa na mbinu zingine. Makala imeonesha kuwa mbinu ya utohoaji inaboresha sarufi ya maneno ili iendane na fonolojia na mofolojia ya lugha ya Kiswahili, huku mbinu ya uhamishaji ikihalalisha maneno kuingia hivyohivyo yalivyo katika lugha nyingine kutokana na ukubalifu wa kifonolojia na wa kimofolojia wa maneno hayo. Zaidi, mbinu ya ukarabati-maneno inazingatia utii wa mazingira ya kitamaduni wa maneno ya Kiswahili katika jamiilugha za kundi F30.

Kwa kuwa utafiti huu ulijikita katika lugha chache tu za Kibantu ambazo ni za Kundi F30, inawezekana kabisa, kutokana na lugha za Kibantu kuwa na asili moja, baadhi ya majina ya Kiswahili ya vitu, hasa vya kitamaduni, yakafanana katika lugha nyingi za Kibantu za kanda tofauti. Tumeona, katika sehemu iliyotangulia, kwamba maneno, mathalani, *kangara* na *makomba*, yameingizwa katika kamusi za Kiswahili, hali inayoonesha kuwa kuna mfanano wa baadhi ya maneno ya kitamaduni katika jamiilugha za makundilugha tofauti ya Kibantu. Kwa sababu

hiyo, makala inapendekeza tafiti za kutosha na za kina kufanyika katika jamiilugha zingine katika kanda zingine za kiisimu, hasa isimu ya Kibantu, ili kubainisha maneno ya Kiswahili yanayotumiwa katika jamii hizo. Ubainishaji huo ufuatiwe na uhakiki wa ukubalifu wa maneno hayo kwa watumiaji na uingizwaji rasmi katika kamusi za Kiswahili zilizopo au kuunda kamusi mahususi. Hatua hii inatarajiwa kuwasaidia watumiaji wengi zaidi wa Kiswahili kuyafahamu maneno hayo, kuyatumia na kukiwezesha Kiswahili kujitajirisha kimsamiati na kuendelea kukua zaidi.

**Marejeleo**

BAKITA (2017) *Kamusi Kuu ya Kiswahili*. Dar es Salaam: Longhorn Publishers.

Bernander, R. (2012) *Contact Induced Change in Bena (G63): A Study of 'Swahilization' in Tanzania Vernacular Language*. Tasinifu ya Umahiri (Haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Gothenburg, Gothenburg.

Habwe, J. na Karanja, P. (2004) *Misingi ya Sarufi ya Kiswahili.* Nairobi: Phoenix Publishers.

Hafez, O. (1996) "Phonological and Morphological Integration of Loanwords into Egyptian Arabic". *Egypte Monde Arabe*, Juz. Na. 27-28: 1-28.

Ismail, J. (2021) "Mchango wa Tasinia ya Sheria katika Ukuzaji na Uenezaji wa Kiswahili Tanzania: Mifano kutoka Mahakama ya Tanzania na Taasisi za Wadau wa Sheria". *East African Journal of Swahili Studies*, Juz. Na. 2(2): 11-22.

Kahigi, K. (2007) "Ujanibishaji wa Office 2003 na Window XP kwa Kiswahili Sanifu". *Kioo cha Lugha*, Juz. Na. 5: 70-99.

Kibwage, A. (2023) *Upanuzi na Ubanaji wa Maana katika Kandanda: Ulinganisho na Ulinganuzi Nchini Kenya na Tanzania*. Tasinifu ya Uzamili (Haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Nairobi, Nairobi.

Kihore, Y., Massamba, D. na Msanjila, Y. (2012) *Sarufi Maumbo ya Kiswahili Sanifu (SAMAKISA): Sekondari na Vyuo.* Dar es Salaam: TUKI.

Kiplimo, C. (2022) "Sababu za Kudondoshwa kwa Sauti za Likwidi katika Maneno Teule". *Editon Consortim Journal of Kiswahili*, Juz. Na. 4 (1): 348-355.

Kiplimo, C. na Mwita, L. (2021) "Thibitisho la Udondoshaji wa Kihistoria wa Fonimu za Likwidi". *East Africa Journal of Swahili Studies*, Juz. Na. 4(1): 43-46.

Legère, K. (2006) "Formal and Informal Development of the Swahili Language: Focus on Tanzania". Katika O.F. Arasanyin na M.A. Pemberton (Wah.), *University of Gothenburg Selected Proceedings of the 36th Annual Conference on African Linguistics*. Somerville, MA, USA: Cascadilla Proceedings Project. Kur. 74-184.

Lehmedi, I. (2021) "Ulinganishi wa Uundaji wa Maneno ya Kiswahili na ya Kiarabu". *Sebha University Journal of Human Sciences*, Juz. Na. 20(2): 52-56.

Lüpke, F. (2016) "Uncovering Small-scale Multilingualism". *Critical Multilingualism Studies*, Juz. Na. 4(2): 34-74.

Maho, J.P. (2009) "The Online Version of the New Updated Guthrie List: A Referential Classification of the Bantu Languages". *NUGL Online*. Inapatikana katika http://goto.glocalnet.net/mahopapers/nuglonline.pdf. Ilisomwa tarehe 27 Mei 2025.

Mgullu, R. (1999) *Mtalaa wa Isimu: Fonetiki, Fonolojia na Mofolojia ya Kiswahili*. Nairobi: Longhorn Publishers.

Moses, M. (2019) *Uchanganuzi wa Kisemantiki-leksia wa Maneno Teule ya Kiswahili wa Maneno Teule ya Kiswahili Yaliyotumika katika Nyimbo Teule Zilizobuniwa na Nonini na Juacali*. Tasinifu ya Uzamili (Haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Maseno, Kisumu.

Mosoto, E. (2016) *Utohozi wa Msamiati kutoka Kiswahili hadi Ekegusii*. Tasinifu ya Uzamili (Haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Nairobi, Nairobi.

Msuya, J. na Mreta, A. (2019) "Adoptation of Loanwords in Chasu". *Journal of Linguistics and Language in Education*, Juz. Na. 13(1): 27-46.

Mwendamseke, F. (2023) "Utohozi wa Nomino za Kiswahili katika Nomino za Kimaswamu". *Journal of Linguistics and Language in Education*, Juz. Na. 17(2): 46-80.

Okal, B. (2012) "Nafasi ya Tafsiri katika Taaluma ya Onomastiki: Uhakiki wa Mbinu Zake katika Tafsiri ya Toponomastiki". *Kiswahili*, Juz. Na. 75: 27-42.

Olson, H. (1964) *The Phonology and Morphology of Rimi*. Connecticut: Hartford Studies in Linguistics.

Philipo, Z. (2022) "Uchapishaji na Usambazaji wa Istilahi za Sayansi Nchini Tanzania: Mifano kutoka Istilahi za Kiswahili za Biolojia, Fizikia na Kemia". *Nuru ya Kiswahili*, Juz. Na. 1(2): 31-58.

Samson, R. (1988) *Ufundi (wa) Magari: Mfano wa Ukuzaji wa Istilahi za Kiswahili Muhimu Tanzania. Matumizi na Usanifishaji Wake*. Tasinifu ya Umahiri (Haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Laiden, Netherlands.

Stephano, R. (2020) "Utoshelevu wa Mawasiliano kwa Kiswahili katika Teknolojia ya SIKANU: Uchunguzi Kifani wa *WhatsApp*". *JULACE*, Juz. Na. 5(1): 1-14.

Stephano, R. (2023) "Mapokezi ya Nomino za Kiswahili katika Ngeli za Nomino za Gɪrɪmi". *Utafiti*, Juz. Na. 8(2): 225-242.

TUKI (2019) *Kamusi ya Kiswahili Sanifu, Toleo la Nne*. Nairobi: Oxford University Press.